

Unashangaa kama unapaswa kupokea chanjo ya COVID-19? Kusita-sita kuhusu chanjo ni jambo la kawaida. Hapa kuna baadhi ya mambo ya kuyazingatia unapokuwa ukifanya uamuzi wako:

1. Dhibiti afya yako!

Kuna uwezekano mkubwa kwamba hutakuwa mgonjwa. Kulingana na CDC*, chanjo hupunguza hatari ya kuambukizwa COVID-19 kwa zaidi ya asilimia 90%.

* Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa

2. Hakuna kukosa tena.

Hata kama umeambukizwa, hakuna haja ya kukarantini ikiwa huna dalili!

3. Kuna utafiti.

Hakuna hatua zilizorukwa au kuharakishwa wakati wa kutengeneza chanjo. Wanasayansi walitumia miongo ya ufahamu wa zamani wa chanjo kuitengeneza kwa haraka na kwa usalama.

4. Fanya tena unachokipenda!

Makampuni mengi yanakuhitaji uchanjwe ili uwe ndani ya majengo na usivae barakoa ukiwa karibu na watu wengine waliochangwa.

5. Linda jamii yako!

Watu wanavyochanjwa zaidi, ndivyo tunavyoweza kurejelea maisha ya kawaida.

6. Usiwe na wasiwasi.

Pumua kwa urahisi ukiwa na amani akilini kwamba umejilinda wewe na wapendwa wako dhidi ya COVID-19.



**Hii ni sindano yako.
Muulize mtoa huduma wako kuhusu jinsi na ni kwa nini unapaswa kupata yako leo!**